# ;JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO**

# HOTUBA YA MHE. DKT. SAADA MKUYA WAZIRI NCHI OFISI YA RAIS, FEDHA NA UCHUMI – ZANZIBAR KATIKA UZINDUZI WA TAARIFA YA UTENDAJI WA SOKO LA BIMA NA MIONGOZO YA BIMA TAREHE 07 OKTOBA, 2022 KATIKA HOTELI YA HYATT REGENCY, KILIMANJARO JIJINI DAR ES SALAAM

**Prof. Florens Luoga, Gavana wa Benki Kuu ya Tanzania,**

**Dkt. Baghayo Saqware, Kamishna wa Bima, Tanzania,**

**Bi. Khadija Said, Naibu Kamishna wa Bima, Tanzania,**

**Wakurugenzi wote wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Nchini,**

**Wakurugenzi wa Kampuni za Bima,**

**Viongozi wa Umoja na Vyama vya Watoa Huduma za Bima Nchini,**

**Wageni waalikwa wote,**

**Ndugu waandishi wa Habari,**

**NAWASALIMU KWA JINA LA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA.**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, Mwingi wa Rehma kwa kutuwezesha na kutupatia kibali cha kufika hapa tukiwa na afya njema**.** Kipekee, napenda kuwashukuru na kuwapongeza viongozi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania, kwanza kwa kuona umuhimu wa kutoa Ripoti ya Utendaji wa Soko la bima nchini. Naambiwa ripoti ya mwaka huu imekuwa na maboresho makubwa. Pili, kuhakikisha wanaishauri Serikali namna nzuri ya kukinga miradi yake ya kimkakati na kuhakikisha shughuli za Wananchi kijamii na kiuchumi zinakingwa na sekta ya bima. Jitihada hizi zina malengo ya kuhakikisha ustawi endelevu wa uchumi kwa mustakabali bora wa Wananchi wetu na vizazi vijavyo.

**Ndugu Washiriki,**

Naamini mnatambua jinsi Serikali ya Mhe. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ilivyodhamiria kuleta maendeleo kwa Wananchi kutokana na mageuzi makubwa yanayoendelea katika sekta zote za uchumi nchini. Serikali imedhamiria kuvutia wawekezaji kwa kupunguza urasimu katika taratibu za kiuwekezaji. Hivyo, shughuli nyingi za kiuchumi na kijamii zinazoendelea nchini zinahitaji sekta ya bima iliyoimara ili kuhakikisha maendeleo yetu ya kiuchumi yanalindwa.

Ni kwa kuzingatia hayo, Serikali imekua ikitunga sheria mbalimbali zinazoweka uhitaji wa bima kwa shughuli za uchumi. Pamoja na Sheria ya Bima na Sheria ya Usalama Barabarani, Mwaka 2017, Serikali kupitia Sheria No. 7 ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali ilianisha maeneo katika kuhakikisha shughuli zote za uchumi zinakingwa na bima. Pia, ninyi ni mashahidi kuwa hivi karibuni Serikali kupitia Sheria ya Fedha Na. 05 ya Mwaka 2022 imeainisha maeneo muhimu manne ili kuongeza wigo wa bima za lazima (*mandatory insurance*) kwa kujumuisha masoko ya umma, majengo ya biashara, bidhaa zote zinazoagizwa kutoka nje, vyombo vya baharini na vivuko. Hatua ambayo inalenga kuimarisha sekta ya fedha jumuishi (*financial inclusion*) na kuongeza matumizi ya bima nchini. Ninalazimika kupitia na kukumbushia hayo ili mtambue ni kwa kiasi gani Serikali inapambana kukuza na kuendeleza sekta ya bima nchini.

**Ndugu Washiriki,**

Ninaamini ripoti nitakayoizindua leo itaonyesha ukuaji wa soko letu la bima kutokana na mabadiliko haya ya sheria. Kwa takwimu za miaka sita yaani kuanzia mwaka 2016-2021, kuonyesha kuwa soko letu limekuwa na wastani wa ukuaji wa asilimia 7%, bado ukuaji huu haujaendana na mchango wa sekta hii muhimu katika pato la taifa kwani takwimu zinaonyesha sekta ya Bima na pensheni mchango wake katika pato la Taifa ni 1.68% tu.

Mchango huu wa sekta ya bima nchini bado unaonekana kuwa mdogo na hauridhishi. Nitaendelea kuwakumbusha kuwa kampuni zote zilizosajiliwa nchini zinawajibika kuonyesha mchango wake katika soko la bima na haswa katika eneo la kubakiza Biashara nchini yaani "local risk retention" hili ni suala muhimu sana katika uchumi wetu. Na kwa kusema hayo naomba nitumie taarifa na takwimu alizozitoa Kamishna hii leo. Inaonekana ubakizaji wa sehemu ya tozo ghafi la bima nchini ni asilimia 55 tu.

Takwimu zinaonyesha kampuni zaidi ya 13 nadni ya soko letu zinategemea bima mtawanyo kwa zaidi ya asilimia hamsini. Hii inatuonyesha kutokuwa tayari kwa kampuni zetu kuhimili majanga ama kutokuwa na mfumo mzuri wa ufanyaji Biashara. Kungekuwa na mfumo mzuri nadha asilimia hizo kampuni zote 13 zilizotawanya zaidi ya 50% ya mapato ghafi yake zisingefanya hivo. Naitaka Mamlaka katika hili la utegemezi mkubwa wa bima mtawanyo kwa kampuni zetu, itekeleze na kusimamia Waraka wake No. 55 kwa ufasaha na miongozo zaidi. Kipekee nitoe pongezi na kuzitambua kampuni tano zenye utegemezi chini ya asilimia 20 wa bima mtawanyo katika soko letu ambazo ni Milembe, BUMACO, Insurance Group of Tanzania, Assemble na Strategis.

**Ndugu Washiriki,**

Taarifa ya Kamishna inaonyesha soko letu limeandikisha kiasi cha tozo ghafi cha Tzs 911,490 bilioni, kiasi ambacho kinaonyesha ukuaji

wa asilimia 10.6% katika mwaka 2021 kutoka tozo ghafi la TZS 824.3 bilioni za mwaka 2020. Pamoja na ongezeko hilo, je tunajua soko letu linapaswa kuwa na thamani gani? Tumeridhika na kiasi tulichonacho kwa sasa? Ni jitihada zipi tufanye kama soko ili kufikia watu wengi na kukuza soko letu?

Haya si tu maswali tunduizi bali yanalenga kuwatoa katika mazoea "Comfort Zone" na kuwa wabunifu ili kupata majawabu katika kukuza faida zitokanazo na undikishaji wa bima, uwekezaji na hata faida baada ya kodi. Najua soko letu kwa sasa liko kwenye mabadiliko ya viwango vya utambuzi wa taarifa za kimahesabu yaani IFSR 17 na hii imeathiri sehemu ya faida kubwa ya uandikishaji kama taarifa inavyoonyesha bahati nzuri taarifa za uwekezaji na faida baada ya kodi ziko chanya hili ni jambo la kujivunia.

**Ndugu Washiriki,**

Serikali imeipa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima malengo mbalimbali ya kukuza sekta ya bima ili kufanikisha azma ya kulinda shughuli za Wananchi kiuchumi na kijamii. Lakini pia, kuhakikisha soko la bima nchini linakuwa sehemu salama na ya kuaminika kwa Wananchi na wawekezaji. Hivyo, kupitia Mpango Mkuu wa Kuendeleza Seka ya Fedha Nchini, Mamlaka imepewa wajibu wa kutekeleza yafuatavyo:

a. Kuhakikisha 10% ya wastaafu wanatumia bidhaa za bima za wastaafu yaani (*Annuities*) ifikapo 2030;
b. Kuhakikisha bidhaa 10 mpya za bima zinazoendana na mahitaji zinaandaliwa ifikapo Mwaka 2030;

c. Kuhakikisha soko linakuwa na njia mpya 8 za usambazaji wa huduma za bima ifikapo 2030;
d. Kuhakikisha idadi ya watanzania wenye bima za maisha inaongezeka;
e. Kuhakikisha 10% ya ada za bima zinatokana na shughuli za kilimo;
f. Kuhakikisha sekta ya bima inatoa na kutengeneza ajira kwa vijana;
g. Kuhakikisha mifumo ya TEHAMA katika sekta ya Bima inakuwa rafiki na kuwiana na mifumo mingine ya sekta ya fedha.

**Ndugu Washiriki,**

Kamishna ametueleza ni kwa jinsi gani Mamlaka wamejipanga na watendaji wake kuendelea kurahisisha ufanyaji biashara na utoaji wa huduma za bima nchini ili kuweza kufikia malengo waliyopewa na Serikali. Pia, leo ninaona miongozo kadhaa imezinduliwa. Kwa kupitia miongozo hii ninatarajia soko litakuwa na kuendelea kuimarika na kuwa soko salama, safi na linalozingatia uweledi.

Lakini naomba niweke msisitizo, ili kuweza kutumia fursa za maendeleo na uwekezaji zinazoibuka kama vile Biashara, shughuli za kilimo, uvuvi, ufugaji maendeleo ya miundombinu, afya, elimu, uchimbaji madini na shughuli zingine za uchumi, Mamlaka inapaswa kuhakikisha huduma za bima zinawafikia Wananchi wengi kwa kuongeza huduma na bidhaa zinazojibu mahitaji ya Wananchi. Taarifa hii inaonyesha ni mikoa saba tu, yaani **Arusha, Mwanza, Unguja, Mbeya, Dodoma, Geita na Morogoro** ndiyo imeweza

kuandikisha tozo ghafi za bima kwa zaidi ya bilioni tano. Hii ukiondoa Dar es Salaam iliyochangia zaidi bilioni 600. Hivyo, nina waagiza wadau wa sekta ya bima kutumia fursa ya za miongozo iliyotolewa na Mamlaka hususani "Sales Force Executives Guideline" kusajili wauza bima maeneo ya pembezoni kama inavyoonyesha taarifa.

**Ndugu Washiriki;**

Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, chini ya Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan imedhamiria kutumia rasilimali zilizopo nchini ili kuboresha na kuinua uchumi wa nchi na Wananchi mmoja mmoja. Hivyo, tuendelee kulisukuma gurudumu hili kwa kuhakikisha shughuli zote za kiuchumi na kijamii zinakingwa na sekta ya Bima. Nitoe wito kwa wataalam wa bima kubuni bidhaa bora za bima ili Wananchi wengi waweze kupata huduma za bima.

**Ndugu Washiriki;**

Nakiri kutambua Mamlaka na soko kwa ujumla lina maombi yake kwa serikali ambayo ni kuteuliwa kwa Bodi ya Taifa ya Bima, kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Bima, Kuanzishwa kwa Skimu ya Taifa ya Bima ya Kilimo na Mifugo na Kuuridhiwa kwa mchakato wa uanzishwaji wa Bodi ya Wataalam wa Bima, Hifadhi ya Jamii na Watakwimu Bima. Haya yote serikali inayatambua na inafuatilia kwa ukaribu ukamilikaji wake.

Na kwa hayo machache natamka rasmi kuwa ripoti ya soko la bima kuanzia 01 Januari 2019 hadi 31st Disemba 2021 imezinduliwa rasmi.

**ASANTENI KWA KUNISIKILIZA**